# Ofisi ya Taifa ya Takwimu

S. L. P 796 Simu: 255- (022) 2122722/3/4 Nukushi:+225 (022)2130852
Dar es Salaam,-TANZANIA Barua pepe: dg@nbs.go.tz

*Unapojibu tafadhali taja:*
Kumb Na: NBS/S.40/21/482

**YALIYOJITOKEZA**

Tarehe: 08 Novemba, 2013

## FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA MWEZI OKTOBA, 2013

## Utangulizi

### Maana ya Fahirisi za Bei za Taifa

Fahirisi za bei za Taifa ni kipimo kinachotumika kupima mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma mbalimbali zinazotumiwa na jamii. Bei za bidhaa na huduma zipatazo 224 hukusanywa kila mwezi kwa kila mkoa nchini.

### Mizania mpya za bidhaa na huduma za jamii na kizio cha bei

Mizania ya Fahirisi za bei za Taifa zimetokana na matumizi ya kaya binafsi kutoka mikoa 21 ya Tanzania Bara. Mizania inajumuisha matumizi ya kaya zote binafsi kutoka mijini na vijijini. Kizio cha Fahirisi za Bei za Taifa kimebadilishwa kutoka Februari 2001=100 hadi Septemba 2010=100.

### Makundi ya bidhaa na huduma za jamii

Marejeo ya Fahirisi za Bei za Taifa yamefanyika kwa kufuata makundi yaliyokubalika Kimataifa yanayoitwa mchanganuo wa matumizi binafsi "Classification of Individual Consumption by Purpose (COICOP)". Fahirisi mpya za Bei inajumuisha makundi 12 ya mfumo wa COICOP pamoja na fahirisi za bei kwa makundi maalumu. Makundi hayo maalumu ni; 1) Vyakula na vinywaji baridi-vikijumuisha vyakula vinavyoliwa majumbani na mahotelini; 2) Nishati na Mafuta - kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli; 3) Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi; 4) Fahirisi za huduma zote za jamii isipokuwa vyakula, vinywaji baridi, nishati na mafuta.

### Namna ya kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa

Maboresho yamefanyika kwenye ukokotoaji wa Fahirisi mpya za Bei za Taifa, ikiwa ni pamoja na kutumia wastani wa jiometria "geometric means" kwenye kukokotoa Fahirisi za Bei katika ngazi za mwanzo badala ya wastani wa kawaida "arithmetic mean", matumizi ya mfumo ulioboreshwa wa ukokotoaji pamoja na mfumo mzima wa kukusanya na kuchambua bei. Kanuni ya "modified Laspeyres index" inaendelea kutumika kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa katika ngazi ya makundi makubwa.

## MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWAKA UMEONGEZEKA HADI ASILIMIA 6.3

### Jedwali Namba 1: Badiliko la Fahirisi za Bei za Taifa kwa Mwezi Oktoba, 2013 (Septemba, 2010 = 100)

| Na. | KUNDI (MAIN GROUP) | Mizania (Weight) | Okt-12 | Sep-13 | Okt -13 | Badiliko la mwezi mmoja | Badiliko la miezi 12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Vyakula na vinywaji baridi | 47.8 | 142.49 | 150.94 | 152.36 | 0.9 | 6.9 |
| 2 | Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku | 3.3 | 127.20 | 140.27 | 140.80 | 0.4 | 10.7 |
| 3 | Mavazi ya nguo na viatu | 6.7 | 124.60 | 130.26 | 130.38 | 0.1 | 4.6 |
| 4 | Nishati, Maji na Makazi | 9.2 | 142.85 | 155.38 | 155.71 | 0.2 | 9.0 |
| 5 | Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba | 6.7 | 123.87 | 127.65 | 127.94 | 0.2 | 3.3 |
| 6 | Gharama za Afya | 0.9 | 105.49 | 108.40 | 108.48 | 0.1 | 2.8 |
| 7 | Usafirishaji | 9.5 | 114.67 | 125.20 | 125.29 | 0.1 | 9.3 |
| 8 | Mawasiliano | 2.1 | 96.43 | 96.58 | 96.59 | 0.0 | 0.2 |
| 9 | Utamaduni na Burudani | 1.3 | 112.32 | 112.94 | 112.87 | -0.1 | 0.5 |
| 10 | Elimu | 1.7 | 110.75 | 113.38 | 113.38 | 0.0 | 2.4 |
| 11 | Hoteli na Migahawa | 6.4 | 130.60 | 133.90 | 134.35 | 0.3 | 2.9 |
| 12 | Bidhaa na huduma nyinginezo | 4.5 | 115.74 | 122.79 | 122.67 | -0.1 | 6.0 |
| **JUMLA – FAHIRISI BIDHAA ZOTE** | | **100** | **132.98** | **140.61** | **141.39** | **0.6** | **6.3** |
| **Makundi Mengine Teule** | | | | | | | |
| 1 | Vyakula—vikijumuisha vyakula vilivyoliwa majumbani na mahotelini | 51.0 | 141.19 | 150.18 | 151.56 | 0.9 | 7.3 |
| 2 | Nishati na Mafuta—kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli | 5.7 | 157.71 | 174.09 | 174.44 | 0.2 | 10.6 |
| 3 | Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi | 49.0 | 123.27 | 130.63 | 130.79 | 0.1 | 6.1 |
| 4 | Fahirisi na huduma zote za jamii Isipokuwa vyakula, nishati na mafuta | 43.3 | 118.09 | 124.63 | 124.77 | 0.1 | 5.7 |

Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa kipimo cha mwaka unapima kiwango cha badiliko la kasi ya bei za bidhaa na huduma zote zinazotumiwa na kaya binafsi. Jedwali namba 1 hapo juu linaonyesha kwamba, Mfumuko wa Bei wa Taifa kwa mwezi Oktoba, 2013 umeongezeka kidogo hadi asilimia 6.3 kutoka asilimia 6.1 mwezi Septemba, 2013. Fahirisi za Bei zimeongezeka hadi 141.39 mwezi Oktoba, 2013 kutoka 132.98 mwezi Oktoba, 2012. Mfumuko wa Bei wa Vyakula na Vinywaji Baridi umeongezeka hadi asilimia 6.9 mwezi Oktoba, 2013 kutoka asilimia 6.5 ilivyokuwa mwezi Septemba, 2013.

### Mfumuko wa Bei kwa Bidhaa za Vyakula na Bidhaa Zisizo za Vyakula

Badiliko la Fahirisi za Bei za bidhaa za vyakula majumbani na migahawani limeongezeka hadi asilimia 7.3 mwezi Oktoba, 2013 ikilinganishwa na asilimia 6.9 mwezi Septemba, 2013. Badiliko la fahirisi za bei kwa bidhaa zisizo za vyakula limeongezeka kidogo hadi asilimia 6.1 mwezi Oktoba, 2013 kutoka asilimia 6.0 mwezi Septemba, 2013.


### Mfumuko wa Bei wa Bidhaa na Huduma Zote Isipokuwa Bidhaa za Vyakula na Nishati

Aina hii ya Fahirisi haijumuishi vyakula vilivyoliwa nyumbani na migahawani, vinywaji baridi, petroli, dizeli, gesi ya kupikia, mafuta ya taa, mkaa na umeme. Vyakula na nishati vina sifa ya

kuwa na bei ambazo hubadilika mara kwa mara hivyo vikiondolewa kwenye Fahirisi ya bidhaa na huduma zote hubakia Fahirisi ambayo ina mwelekeo imara kwa Watunga Sera.

Mfumuko wa Bei ambao haujumuishi vyakula na nishati kwa mwezi wa Oktoba, 2013 umepungua hadi asilimia 5.7 ikilinganishwa na asilimia 5.8 mwezi Septemba, 2013.

**Kielelezo Namba 1: Mwenendo wa Fahirisi za Bei za Taifa na Mfumuko wa Bei Kutoka Oktoba, 2012 Hadi Oktoba, 2013. (Septemba 2010 = 100)**




Kielelezo Namba 1 hapo juu kinaonyesha kuwa, katika kipindi kati ya mwezi Oktoba, 2012 hadi Oktoba, 2013, Fahirisi za Bei zimeonyesha mienendo tofauti. Kumekuwa na mwenendo wa kuongezeka kwa bei za bidhaa na huduma mbalimbali kutoka mwezi Oktoba 2012 hadi mwezi Aprili, 2013 na mwenendo imara wa Fahirisi za Bei kutoka mwezi Mei, 2013 hadi mwezi Oktoba, 2013. Mfumuko wa Bei umekuwa na mwenendo wa kushuka kutoka asilimia 12.9 mwezi Oktoba, 2012 hadi kufikia asilimia 6.1 mwezi Septemba, 2013 na kuongezeka kidogo hadi asilimia 6.3 mwezi Oktoba, 2013.

## MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWEZI UMEONGEZEKA KWA ASILIMIA 0.6

Mfumuko wa Bei wa mwezi Oktoba 2013 umeongezeka kwa asilimia 0.6 ikilinganishwa na asilimia 0.5 mwezi Septemba 2013. Fahirisi za Bei zimeongezeka hadi 141.39 mwezi Oktoba, 2013 kutoka 140.61 mwezi Septemba, 2013. Ongezeko la fahirisi limechangiwa na kuongezeka kwa bei za bidhaa za vyakula na bidhaa zisizo za vyakula. Baadhi ya bidhaa za vyakula zilizochangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa fahirisi ni; unga wa mahindi kwa asilimia 1.5, unga wa muhogo kwa asilimia 3.5, nyama kwa asilimia 1.2, kuku kwa asilimia 3.7, samaki wabichi kwa asilimia 4.1, samaki wakavu kwa asilimia 9.0, dagaa kwa asilimia 2.5, maziwa ya ng'ombe (fresh milk) kwa asilimia 1.2, matunda kwa asilimia 2.9, nazi kwa asilimia 2.6, viazi vitamu kwa asilimia 4.2 na asali kwa asilimia 5.0. Bidhaa zisizo za chakula zilizochangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa fahirisi ni; mavazi ya watoto kwa asilimia 0.4, mafuta ya taa kwa asilimia 2.1 na vifaa vya nyumbani vya usafi kwa asilimia 0.4.


## Thamani ya Shilingi ya Tanzania Mwezi Oktoba, 2013 Ikilinganishwa na Mwezi Septemba, 2010

**Tafsiri**: Thamani ya Shilingi ya Tanzania inatafsiriwa kuwa ni badiliko la Uwezo wa Shilingi ya Tanzania katika kununua bidhaa na huduma zilezile za mlaji ambazo Shilingi ya Tanzania ingeweza kununua katika vipindi tofauti. Ikiwa wastani wa Fahirisi za Bei za Taifa unaongezeka, Uwezo wa Shilingi ya Tanzania katika kununua bidhaa na huduma hupungua.

Uwezo wa Shilingi 100 ya Tanzania katika kununua bidhaa na huduma umepungua hadi Shilingi 70 na senti 73 mwezi Oktoba 2013 kutoka mwezi Septemba, 2010.

## MIENENDO YA BEI

### Kielelezo Namba 2: Mienendo ya Bei kwa Makundi Mbalimbali ya Fahirisi za Bei Kutoka Oktoba, 2012 Hadi Oktoba, 2013. (Septemba 2010 = 100)




Kielelezo Namba 2 hapo juu kinaonyesha mienendo ya bei kwa makundi mbalimbali ya fahirisi za bei kuanzia mwezi Oktoba, 2012 hadi mwezi Oktoba, 2013. Kwa wastani, Fahirisi za nishati na mafuta na Fahirisi za vyakula na vinywaji baridi zimekuwa na mwenendo wa juu kwa kipindi chote zikilinganishwa na fahirisi zingine. Kundi la nishati na mafuta limeonyesha pia kuwa na mwenendo wa fahirisi usio imara ikilinganishwa na makundi mengine kwa kipindi husika. Fahirisi za bidhaa zisizo za chakula na fahirisi za bidhaa zisizo jumuisha chakula pamoja na nishati zimeonesha mwenendo wa bei ulio imara.

Ofisi ya Taifa ya Takwimu itatoa Mfumuko wa Bei wa Taifa wa mwezi Novemba, 2013 tarehe 08 Desemba, 2013. Kwa maoni ya kuboresha taarifa hii wasiliana na;

**Mawasiliano: Mkurugenzi Mkuu,**
**Ofisi ya Taifa ya Takwimu**